

TANZANIA / JUDGMENT

tausi masudi vs musa ally others

2023 tzhc 22899 4 agosti 2023

COURT
TZHCDECIDED
1 January 2023

Source: media.tanzlii.org · Research copy typeset by Esheria. Not court-issued or certified.

KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA KANDA YA TABORA RUFAA YA JINAI NAMBA 1 YA 2022 (Inatokana na shauri la Awali la Jinai Namba 19/2021 katika Mahakama ya Mwanzo Isevy na shauri la Rufaa No. 04 la 2021 katika Mahakama ya Wiiaya Tabora) TAUSI MASUDI..... —..... —----- MWOMBA RUFAA DHIDIYA MUSSA ALLY----- MJIBU RUFAA WA 1 TINGI ALLY..... MJIBU RUFAA WA 2 TATU JUMANNE.....MJIBU RUFAA WA 3 HUKUMU Date: 17/07/2023 & 04/08/2023

BAH ATI SALEM A, J.: Wajibu rufaa tajwa hapo juu Mussa Ally, Tingi Ally na Tatu Jumanne walishitakiwa katika Mahakama ya Mwanzo Isevy mjini Tabora wakikabiliwa na shitaka moja la Shambulio la kudhuru mwili dhidi ya kifungu namba 241 cha Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 iliyorejelewa mwaka 2019. Katika maelezo ya kosa kwa mujibu wa hati ya mashtaka ilielezwa kuwa, mnamo tarehe 12/01/2021 majira ya saa 07:00hrs huko maeneo ya Lusange Kata ya Ntalikwa Manispaa ya Tabora kwa makusudi na bila halali washtakiwa wote watatu walimshambulia Tausi Masudi kwa kumpiga na fimbo maeneo mbalimbali ya mwili wake na kumsababishia maumivu makali huku wakijua kufanya hivyo ni kosa na kinyume na sheria. i Washtakiwa waliposomewa shitaka wote walikana ndipo shauri liliposikilizwa na baadae mjibu rufaa wa 1 alipatikana na hatia kisha kuhukumiwa kulipa faini ya shilingi za kitanzania laki mbili (200,000/=) au kifungo cha miezi 6 gerezeni endapo atashindwa kulipa faini; pia Mahakama ilimwamuru mjibu rufaa namba 1 kumlipa mwomba rufaa fidia ya shilingi za kitanzania elfu Hamsini (50,000/=) ikiwa ni gharama alizotumia katika matibabu. Mwomba rufaa hakuridhika na uamuzi huo wa Mahakama hivyo aiikata rufaa katika Mahakama ya wilaya kupitia Shauri la rufaa Namba 4/2021 akipinga kuachiliwa huru kwa mjibu rufaa namba 2 na namba 3 na pia alipinga adhabu iliyotolewa kwa mjibu rufaa namba 1 kuwa ni ndogo ukilinganisha na ukubwa wa kosa alilolitenda. Shauri la rufaa katika Mahakama ya Wilaya lilisikilizwa na baada ya Mheshimiwa Hakimu kupitia nyaraka zilizowasilishwa katika shauri la awali aligundua kwamba Kielelezo Al ambayo ni Fomu ya Polisi namba 3 (PF3) ilijazwa tarehe tofauti na tarehe ya siku ambayo ilisemekana kuwa mwomba rufaa alifikishwa hospitali kufanyiwa ukaguzi wa kitabibu. Ulikuwa ni msimamo wa Hakimu kuwa tofauti hiyo ilitia Mashaka katika ushahidi wa upande wa jinai hivyo kwa sababu hiyo alitupilia mbali rufaa na kuendeleza uamuzi wa Mahakama ya Mwanzo. Mwombaji bado hakuridhika na uamuzi uliotolewa na Mahakama ya Wilaya, aiikata rufaa katika Mahakama hii akieleza sababu tano zilizomfanya akate rufaa hii, alieleza: -

1. Kwamba Hakimu Mkazi alikosea kisheria na kimantiki kwa kuendeleza maamuzi ya Mahakama ya Mwanzo kuwa shitaka halikuthibitishwa dhidi ya mjibu rufaa wa 2 na wa 3. 2
2. Kwamba Mheshimiwa Hakimu alikosea kisheria kwa kutokuzingatia ushahidi kwamba tarehe 12/01/2021 washitakiwa wote kwa makusudi walimshambulia mwombaji.
3. Kwamba Hakimu Mkazi alikosea kisheria na kimantiki kwa kuendeleza adhabu ndogo na fidia ndogo ukilinganisha na madhara yaliyosababishwa na wajibu rufaa kwa makusudi.
4. Kwamba Hakimu msomi alikosea kisheria na kimantiki kwa kuwaachilia huru mjibu rufaa wa 2 na wa 3 ilhali majeraha yaliyoelezwa katika kielelezo Al yalisababishwa na washtakiwa wote watatu.
5. Kwamba Hakimu alikosea kisheria na kimantiki kwa kutokuzingatia ushahidi kwamba kulikuwa na njama kati ya washtakiwa wote watatu kama inavyoonekana katika rekodi kwamba wote walienda kwa pamoja katika eneo la tukio kutenda kosa la jinai. Ni kupitia sababu hizo mwombaji anaiomba Mahakama itupilie maamuzi ya Mahakama mbili za chini kuhusiana na kuachiliwa huru kwa wajibu rufaa namba 2 na 3 kisha kuwapata na hatia kwa mujibu wa shitaka waliloshitakiwa nalo; pia anaiomba Mahakama iongeze adhabu iliyotolewa kwa mjibu rufaa namba 1 ikiwa ni pamoja na nyongeza ya fidia iliyotolewa. Shauri hili lilipoitwa kwa ajili ya kusikilizwa mwombaji alikuwepo yeye mwenyewe na wajibu maombi wote hawakufika hivyo rufaa ilisikilizwa upande mmoja. Katika mawasilisho yake, mwombaji alieleza Mahakama kuwa, Mahakama za chini ilikosea kwa kuamua kwamba shitaka dhidi ya wajibu rufaa namba 2 na 3 halikuthibitishwa pasi na kuacha shaka ilhali yeye 3 alilazwa hospitali na washtakiwa kukamatwa. Pia alieleza kwamba yeye alienda hospitali tarehe 15 lakini PF3 inaonesha kwamba ni tarehe 12. Mwombaji aliongeza kwamba fidia iliyoamuriwa na Mahakamani ndogo sana ukilinganisha na madhara aliyopata; pia anashangaa ni kwanini mjibu rufaa namba 2 na namba 3 waliachiliwa huru. Nikianza na hukumu iliyotolewa katika Mahakama ya Mwanzo Isevyi inaonyesha kwamba msingi wa maamuzi ya mheshimiwa Hakimu ulijikita katika Fomu ya Polisi (PF3) kwa kuzingatia maoni ya daktari, nitanukuu "kutokana na maelezo ya mlalamikaji kwamba alipoteza fahamu na kushituka saa 7 mchana akiwa hospitali Remarks za daktari anasema mlalamikaji alipata mshtuko kwenye ubongo Hiyosababisha kupoteza fahamu na maumivu yaliyotokana na shambuHo na kupata dawa za maumivu" Nimeamua kupitia Kielelezo Al ambacho ni PF3 nimeona kwamba hakionyeshi kilitolewa na kituo gani cha polisi wala, hakionyeshi namba ya lalamiko lililofunguliwa polisi na wala hakionyeshi kosa lililolalamikiwa. Pia katika mawasilisho ya mwombaji katika Mahakama hii alieleza kwamba yeye alifika hospitali tarehe 15/01/2021, maelezo hayo yanakinzana na ushahidi wake mwenyewe alioutoa katika Mahakama ya Mwanzo kwamba siku ya tukio tarehe 12/01/2021 alipoteza fahamu na kuzinduka saa saba mchana akiwa katika Hospitali ya Kitete. Tofauti zote hizi zinakifanya kielelezo Al kuwa batili na kukosa nguvu ya ushahidi kuthibitisha yale yote aliyoyaeleza mwomba rufaa. Nashangaa ni kwanini mahakimu wa ngazi zote mbili hawakuyaona makosa hayo katika rekodi za Mahakama. 4 Jambo lingine ambalo nimeliona la muhimu kuzingatiwa na Mahakama hii juu ya namna ambavyo Mahakama za Mwanzo zinatoa

maamuzi yake pale zinapokaa na washauri wa Mahakama. Kifungu cha 7

- (1) na (2) cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu Sura ya 11 [R.E 2019] kama kilivyokuwa kinatumika wakati huo kilielekeza kwamba, nitanukuu; "7(1) katika kiia mwenendo katika Mahakama ya Mwanzo, ikijumuisha utoaji wa maamuzi, Mahakama itaketi na washauri wasiopungua wawiii
- (2) Mambo yote katika Mahakama ya Mwanzo ikiwa ni pamoja na maamuzi katika suaia ioiote, swaia ia kuahirisha usikiiizwaji, maombi ya dhamana, suaia ia hatia au kutokuwa na hatia kwa mtuhumiwa yeyote, uamuzi wa adhabu, tathmini ya tuzo yoyote ya fedha na masuaia yoyote ambayo, iwapo kutatokea tofauti kati ya hakimumu na washauri au yeyote kati yao, yataamuiwa kwa kura ya waiio wengi kati ya mahakimu na washauri waiiopo na ikitokea kura za usawa hakimumu atakuwa na kura turufu pamoja na kura yake ya awaia". Rekodi za shauri la awaia katika Mahakama ya Mwanzo zinaonyesha kwamba katika shauri hilo kulikuwa na washauri wawiii wa Mahakama na baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili walitoa maoni yao kama ifuatavyo. Nitanukuu "Muntaz Hussein 5 Washtakiwa hawana hatia kwa sababu Mahakama Hifika kwenye eneo la tukio ambapo alipokuwa mlalamikaji anangda mbegu Mahakama Hikuta hapakuwa na dalili ya kuwa na mbegu, pia maelezo ya daktari hayakuonyesha kwamba kulikuwa na mpasuko wowote ule wa kuchuruzika damu, Hionyesha maumivu ya kawaida. Sahihiya mshauri (imesainiwa)" "Rehema John Nami naungana na mshauri mwenzangu washtakiwa hawana hatia kwa sababu mlalamikaji alieleza kuwa alikutwa anang'oa mbegu na Mahakama Hipoenda kwenye tukio palikuwa hakuna dalili ya mbegu, pia PF3 ya daktari imeonyesha kuwa hakuna shambulio la kudhuru mwi/i Sahihiya mshauri (imesainiwa)" Kwa mujibu wa maoni yaliyotolewa na washauri wa Mahakama na kwa kuzingatia maelekezo ya sheria kama yalivyonukuliwa kutoka kifungu cha 7 cha sheria ya Mahakama za Mahakimu Sura ya 11 [R.E 2019] ni wazi kwamba maamuzi sahihi ya Mahakama yalitokana na maoni yaliyotolewa na wauri kwamba washtakiwa wote hawana hatia. Kwa kuwa uamuzi wa Hakimumu ulikiuka kifungu cha 7(1) na (2) cha sheria kwa kutokuzingatia maoni ya washauri ambayo kimsingi kura 2 kati ya 3 zilizotakiwa kuamua maamuzi yale zilishauri kwamba washtakiwa wote hawana hatia. 6 Kwa msingi huo hukumu ya Mahakama ya Mwanzo iliyomtia hatiani mjibu rufaa namba 1 na kisha kumpa adhabu ilikuwa ni batili kwa sababu ilikiuka mwongozo wa sheria katika kifungu cha saba tajwa hapo juu. Kwa sababu zilizotajwa katika hukumu hii, natamka kwamba hukumu ya Mahakama ya Mwanzo na ya Mahakama ya Wilaya zinafutwa na rufaa hii inatupiliwa mbali. Haki ya kukata rufaa imeelezwa. A. BAHATI SALEMA JAJI 04/08/2023 7

Source & reproduction note

Judgment wording, source notices and original paragraph numbers are retained. Esheria supplies the layout and this PDF's page numbers; these are not the source pagination. This is a research copy, not an official or certified court document. Check quotations, citations and publication restrictions against the original source before relying on it.

ORIGINAL SOURCE https://media.tanzlii.org/media/judgment/305776/source_file/tausi-masudi-vs-musa-ally-others-2023-tzhc-22899-4-agosti-2023.pdf

CASE PAGE <https://chat.esheria.ai/case-law/tanzania/tausi-masudi-assault-tzhc-2023--6a3ea52d3b1caa912982641c>

Prepared on 14 October 2026 · Esheria